

*Mulika, Na. 43 (1), 98-116
Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

Ujitokezaji wa Ruwaza ya Shujaa wa Kiafrika katika Kisakale cha Mukwavinyika wa Jamii ya Wahehe

*Aneth Kasebele¹
Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

DOI: <https://doi.org/10.56279/mulika.na43t1.6>

Ikisiri

Makala haya yamechunguza ujitokezaji wa ruwaza ya shujaa wa Kiafrika katika Kisakale cha Mukwavinyika wa jamii ya Wahehe. Tafiti tangulizi zinaonesha kuwa tendi na hadithi nyingi za mashujaa duniani huwa na ruwaza fulani inayofanana na safari yao (mashujaa) hupitia karibu hatua zilezile. Suala hili linatupatia muundo wa msingi ambao ni wa kiulimwengu na wenyewe kutabirika. Hata hivyo, suala hilo limeibua maswali kama vile: je, kama ruwaza za mashujaa kote ulimwenguni zinafanana, jamii hizo zinafanana pia? Kama hazifanani, je, jamii zinazotofautiana katika nyanja mbalimbali za maisha zinawezaje kuwa na ruwaza za mashujaa zinazofanana kwa kila hali? Hivyo, kilichofanyika katika makala haya ni kubainisha ruwaza ya shujaa kama inavyojitokeza katika Kisakale cha Mukwavinyika ili kubaini umbile lake ni la namna gani. Katika kufanikisha hilo, makala haya yameongozwa na Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa kwa mujibu wa Raglan (1934). Aidha, data zake zimekusanywa kwa njia ya usaili na uchambuzi matini kutoka katika kijiji cha Kalenga kilichopo mkoani Iringa. Makala haya yamebaini kuwa ruwaza ya shujaa iliyojitokeza katika Kisakale cha Mukwavinyika ina hatua 15 alizopititia shujaa katika makuzi yake. Pia, imebainika kuwa mashujaa wa Kiafrika wana ruwaza zenye vipengele vinavyofanana na vinavyotofautiana na vyta mashujaa wengine ulimwenguni.

1.0 Utangulizi

Historia inaonesha kuwa kuna mashujaa wanaume na wanawake wa aina mbalimbali ulimwenguni. Miogoni mwa mashujaa hao ni wa kijadi, kihistoria na wa kidini. Kwa mfano, Hook (1991) anataja mashujaa kuanzia kwa Mwanamwini (Finland), Mfalme Arthur (Uingereza), Buddha (India), Napoleon (Ufaransa), Martin Luther (Udachi), Lenin (Urusi) na Mao TseTung (China). Sifa moja kuu ya mashujaa hao anayoitaja Hook ni kuwa waasisi wa mfumo na mtindo mpya wa maisha ya jamii na pengine ni waasisi wa mataifa mapya ambayo hayakuwapo

¹ Baruapepe: aneth.kasebele@muce.ac.tz

kabla. Hawa ni watu ambao maisha na matendo yao yaliubadilisha mwelekeo wa jamii zao na wa ulimwengu kwa ujumla. Suala kuhusu kuwapo kwa shujaa wa Kiafrika liliibua mjadala mkubwa mionganii mwa wanazuoni. Mjadala huo ni mionganii mwa masuala yaliyoibua kile kinachoitwa Mkanganyiko katika Utendi wa Kiafrika (yaani, *African Epic Controversy*) (taz. Mulokozi, 2002). Mkanganyiko huu ulikuwa maarufu sana kuanzia miaka ya 1970 na kuendelea ambao unatokana na kuwapo kwa makundi mawili ya wanazuoni. Wapo wanaoona kuwa hakuna shujaa wa Kiafrika na wale wanaoamini kwamba kuna shujaa wa Kiafrika. Wanaoamini kutokuwapo kwa shujaa wa Kiafrika ni pamoja na Bowra (1952), Finnegan (1970) na Knappert (1983).

Kama anavyoeleza Mulokozi (2002), mawazo ya wataalamu hao yaliwachochea watafiti wa Kiafrika kuanza kutafiti kuhusu kuwapo kwa kipera cha utendi na mashujaa wake katika bara la Afrika. Mionganii mwa watafiti hao ni pamoja na Okpewho (1979), Kunene (1980), Seydou (1983), Mbele (1986) na Mulokozi (1999). Matokeo ya tafiti zao yamedhihirisha kuwa Afrika kuna tendi na pia kuna mashujaa ambao wana sifa kadhaa zinazojidhihirisha. Mionganii mwa wanaotajwa katika maandiko mbalimbali kuwa mashujaa wa Kiafrika ni pamoja na Shaka Zulu (Wazulu) (taz. Mofolo, 1975), Sundiata (Wamande) (taz. Johnson, 1978), Mwindo (Wanyanga) (taz. Okpewho, 1979), Lianja (Wamongo) (taz. Kunene, 1980), Fumo Liyongo (Waswahili) (taz. Mulokozi, 1999) na Rukiza na Kachwenyanja (Wahaya) (taz. Mulokozi, 2002). Hata hivyo, Samwel (2015) anabainisha kuwa kwa sasa mkanganyiko kuhusu kuwapo kwa mashujaa na utendi katika jamii za Kiafrika umepungua kwani tafiti hizo zimethibitisha kuwa Afrika kuna tendi, pia kuna mashujaa wanaosawiriwa kupitia tanzu mbalimbali za fasihi.

Aidha, watafiti wa Kiafrika walipiga hatua na kubainisha sifa mbalimbali za mashujaa hao zinazoonekana katika jamii za Kiafrika. Pia, walibainisha ruwaza za mashujaa hao wa jamii za Kiafrika. Kimsingi, ruwaza inajikita katika hatua mbalimbali za ukuaji wa shujaa tangu kuzaliwa, kusafiri nchi za mbali, kufundwa, kukomaa, kurejea na kupata ushindi (Mulokozi, 2017). Hatua hizi za ukuaji wa shujaa zimeelezwa katika viunzi vya watafiti mbalimbali waliotafiti mashujaa wa Kiafrika na mashujaa wengine ulimwenguni. Hata hivyo, kwa kuwa mashujaa hutoka katika jamii tofautitofauti ulimwenguni zenye tamaduni na falsafa tofauti zinazoweza kusababisha ruwaza za mashujaa kufanana na kutofautiana. Hivyo, kilichofanyika katika makala haya ni kuchunguza ujitekezaji wa ruwaza ya shujaa wa Kiafrika kama inavyosawiriwa katika kisakale chake ili kubaini umbile lake ni la namna gani.

2.0 Muhtasari wa Kisakale cha Mukwavinyika

Kisakale cha “Mukwavinyika” kinamhusu shujaa huyo aliyejikuwa mtoto wa mtawala wa jamii ya Wahehe aitwaye Munyigumba. Mukwavinyika alikabidhiwa utawala katika jamii ya Wahehe tangu akiwa kijana mdogo mara baada ya baba

yake mzazi kufariki dunia. Mukwavinyika alikuwa mtawala aliyependwa sana na watu wake kutokana na kuwawezesha kuwashinda maadui zao. Aidha, kila walipojitokeza maadui kupambana naye, wanajamii walijitokeza kwa wingi kumsaidia katika jeshi lake. Vilevile, baba yake mzazi aitwaye Munyigumba aliendelea kumlinda na kumpigania Mukwavinyika hata kama alikuwa ameshafariki dunia. Kwa mfano, wakati mmoja, Mwambambe aliyejewa mfuasi na mlinzi wa baba yake Mukwavinyika alifanya mapinduzi na kuchukua madaraka kinguvu kisha akaunda mpango mzima wa kumuua Mukwavinyika. Kutokana na hayo aliyojafanya Mwambambe, Mukwavinyika aliona ni bora kutoroka na kwenda kuishi Ugogoni kuliko kubaki Uheheni alikokuwa anakumbwa na hofu ya kifo. Hata hivyo, huko Uheheni, Wahehe waliupinga utawala wa Mwambambe kwa sababu ulikuwa utawala wa kikatili sana. Hivyo, Wahehe walifanya shauri la siri wakamwita Mukwavinyika aje kupigana vita na Mwambambe kwa lengo la kumtoa Mwambambe madarakani. Vita katika ya Mwambambe na Mukwavinyika vilikuwa vikali sana kwa sababu Mwambambe alikuwa mtu mwenye nguvu za ajabu. Mwambambe, kila aliporushwa mikuki mwilini, ilikuwa inamchoma lakini hakufa, badala yake aliichomoa na kuwatupia wanajeshi wa Mukwavinyika huku akia watu zaidi ya kumi kwa wakati mmoja.

Usiku mmoja, Mukwavinyika alipokuwa amelala, alitembelewa na baba yake mzazi katika ndoto akimweleza mbinu za kutumia ili kumuua Mwambambe. Alimweleza kwamba ili Mwambambe afe anatakiwa kuchomwa mkuki katika kisigino na kwenye dole gumba. Baada ya kuijua mbinu hiyo, mfuasi wa Mukwavinyika aitwaye Mkimayena alimchoma mkuki Mwambambe kama ilivyoelekezwa. Baada ya kuchomwa mkuki, Mwambambe alianza kuhisi kichefuchefu na akaanguka chini kama gunia, kisha akakata roho. Wafuasi wa Mukwavinyika walipoona Mwambambe amekufa, walimkatakata vipandevipande na kumla nyama palepale huku ikiwa mbichi.

Kisakale cha “Mukwavinyika” kinaleza pia kuwa Mukwavinyika alikuwa kiongozi tajiri na mwenye wake wengi waliofika sitini na mbili. Kutokana na hilo, Mukwavinyika alikuwa na watoto wengi. Shujaa huyo kila alipomwona mwanamke mzuri alimchukua kuwa mke wake, na wanawake hao hawakuruhusiwa kuwa na wanaume wengine. Ili kuhakikisha kuwa wake zake hawaendi nje ya ndoa, Mukwavinyika alikuwa na nguvu za kiganga zilizomsaidia kutambua mwanamke aliyeenda nje ya ndoa na hivyo kumchukulia hatua. Kutokana na hilo, wake zake walijitahidi sana kuwa waaminifu. Vilevile, Mukwavinyika aliogopwa sana na watu wake kutokana na kuwa na nguvu nyingi za kiganga zilizomwezesha si tu kushinda vita, bali pia kuwabaini maadui zake katika utawala wake. Hili lilimsaidia Mukwavinyika kudumu katika utawala wa jamii ya Wahehe.

Kisakale hicho kinaleza kuwa utawala wa Mukwavinyika ulikuwa wenye nguvu kwa sababu Mukwavinyika alipanua utawala wake katika eneo kubwa mpaka nje ya

mipaka ya Uhehe. Pia, Mukwavinyika aliimarisha utawala wake kwa kujenga ngome kubwa katika kijiji cha Kalenga kilichopo ndani ya wilaya ya Iringa Vijiini. Baada ya Mukwavinyika kuweka makazi yake rasmi katika kijiji cha Kalenga, kijiji hicho kilikua na kupata sifa. Kisakale hicho kinaendelea kueleza kuwa katika kipindi hiki ambacho Mukwavinyika alikuwa anaimarisha ngome yake huko Kalenga, Wajerumani walikuwa wamekwishaangia Tanganyika wakiwa wanapanua utawala wao. Wajerumani walikuwa na mashaka na Mukwavinyika kwa sababu walishasikia kuwa ni mfalme mwenye nguvu na hodari katika vita. Hivyo, mara kwa mara, Mukwavinyika na Wajerumani waliingia vitani. Katika vita vya kwanza, Mukwavinyika alishinda kwa kuwaua askari wengi wa Kijerumani huko Lugalo. Hata hivyo, katika vita vya mara ya pili, Mukwavinyika alishindwa, akazidiwa nguvu na akakimbia kwenda kujificha katika pango huko Mulambalasi. Mukwavinyika alipokuwa huko Mulambalasi alijiua kwa kujipiga risasi ili asikamatwe na Wajerumani. Walipofanikiwa kufika mahali alipojificha Mukwavinyika, Wajerumani walikuta ameshafariki dunia. Hivyo basi, Wajerumani waliamua kukikata kichwa cha Mukwavinyika kwa ajili ya kwenda kumwonesha gavana wao. Huo ndio ukawa mwisho wa maisha ya shujaa Mukwavinyika Munyigumba Mwamuyinga wa jamii ya Wahehe.

3.0 Nadharia na Methodolojia ya Utafiti

Sehemu hii imefafanua msingi wa kinadharia na mbinu mbalimbali za utafiti zilizotumika katika makala hii kama ifuatavyo:

3.1 Nadharia

Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa iliyoasisiwa na Lord Raglan (1934) kwa sababu shujaa anayechunguzwa anatoka katika jamii za kijadi za Kiafrika kama alivyofanya Raglan alipotafiti mashujaa wa kijadi kutoka katika jamii za Kimagharibi hasa Ugiriki. Kwa mujibu wa Raglan (1934) shujaa anapitia hatua 22 katika makuzi yake kama ifuatavyo: mosi, mama yake ni binti mfalme bikira; pili, baba yake ni mfalme; tatu, aghalabu ni ndugu wa karibu wa mama yake, lakini; nne, mazingira ya kutungwa mimba yake ni ya kimazingara, na; tano, inasemekana kuwa ni mwana wa Mungu; sita, anapozaliwa linafanywa jaribio aghalabu na baba yake la kumuua, lakini; saba, anatoroshwa kwa siri, na; nane, analelewa na wazazi wa kambo katika nchi ya mbali; tisa, hatuambiwi chochote kuhusu utoto wake, lakini; kumi, anapokua anarejea au anakwenda katika ufalme wa baadaye; kumi na moja, baada ya ushindi dhidi ya mfalme na/au jitu, joka, au mynyama mkali; kumi na mbili, anamwoa binti mfalme, aghalabu binti ya mtangulizi wake, na; kumi na tatu, anakuwa mfalme; kumi na nne, kwa muda fulani anatawala bila mkasa; kumi na tano, anatunga sheria; kumi na sita, baadaye anakataliwa na miungu na/au raia zake; kumi na saba, anaondolewa katika kitie chake cha enzi na kufukuzwa mjini; kumi na nane, anakufa kimazingara (kiajabuajabu); kumi na tisa, aghalabu juu ya kilima; ishirini, wanawe kama wapo hawamrithi; ishirini na moja,

mwili wake hauzikwi, hata hivyo; ishirini na mbili, anakuwa na madhabahu moja au zaidi za matambiko yake.

3.2 Methodolojia ya Utafiti

Data za utafiti huu zilikusanywa uwandani mkoani Iringa katika kata ya Kalenga kuanzia mwaka 2020 mpaka 2021. Mkoa wa Iringa uliteuliwa kwa sababu ndio mkoa ambao jamii kubwa ya Wahehe inaishi. Pia, kata ya Kalenga iliteuliwa kwa sababu ndipo panapoelezwa kuwa aliishi shujaa Mukwavinyika. Aidha, katika kata ya Kalenga kuna Makumbusho ambayo kwayo nyaraka mbalimbali zinazohusu maisha ya shujaa Mukwavinyika zimehifadhiwa. Hivyo, katika kata hiyo, mtafiti alipata historia ya kina kumhusu shujaa Mukwavinyika ambaye pia anarejelewa katika kisakale. Katika ukusanyaji wa data, mtafiti alitumia mbinu ya usaili na uchambuzi matini. Mtafiti alifanya usaili wa ana kwa ana na watoataarifa 9. Pia, alifanya usaili kwa kutumia njia ya simu kwa watoataarifa 3 ambao hawakuwapo uwandani kwa sababu walisafiri kwenda katika kata zingine kwa shughuli za kilimo. Mbinu ya usaili ilimsaidia mtafiti kukusanya data za kutosha zilizosaidia kufafanua ujitokezaji wa ruwaza ya shujaa wa Kiafrika katika Kisakale cha Mukwavinyika wa jamii ya Wahehe.

Pia, mbinu ya uchambuzi matini iliteuliwa ili kukusanya data ambazo hazikuweza kukusanywa kwa kutumia njia ya usaili. Matini zilizochambuliwa ni zile zinazohusu historia ya jamii ya Wahehe, simulizi za kifasihi na zisizo za kifasihi kuhusu shujaa Mukwavinyika. Kwa upande wa uchambuzi wa data, mtafiti alianza kwa kunukuu masimulizi kuhusu Kisakale cha Mukwavinyika. Kwa kufanya hivyo, mtafiti aliweka data za masimulizi katika maandishi. Hatua iliyofuata, mtafiti alibainisha data za utafiti huu kulingana na lengo la makala haya. Baada ya kubainisha data, hatua iliyofuata, mtafiti alichambua data kwa kuhusisha na mihimili ya Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa kwa mujibu wa Raglan (1934). Hatua ya mwisho, mtafiti alichambua na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Mkabala wa kitaamuli, unaolenga kuchambua na kuwasilisha data kwa njia ya maelezo, ndio uliotumika katika utafiti huu. Kwa kutumia mkabala huu, uchambuzi na uwasilishaji wa data ulifanyika ili kuonesha ujitokezaji wa ruwaza ya shujaa wa Kiafrika katika Kisakale cha Mukwavinyika wa jamii ya Wahehe.

4.0 Ujitokezaji wa Ruwaza ya Shujaa wa Kiafrika katika Kisakale cha Mukwavinyika

Sehemu hii imechambua ruwaza aliyoipitia shujaa Mukwavinyika katika makuzi yake tangu alipozaliwa mpaka alipofariki dunia. Kupitia ruwaza hiyo, tunabainisha ruwaza ya shujaa kama inavyojitokeza katika Kisakale cha Mukwavinyika.

4.1 Baba yake Shujaa ni Mfalme

Hatua ya kwanza ya ruwaza ya shujaa inayojibainisha katika Kisakale cha Mukwavinyika ni baba mzazi wa shujaa kuwa mfalme. Suala la baba mzazi wa

shujaa kuwa mfalme limefungamana pia na mawazo yaliyotolewa na Raglan (1934) kuwa baba wa shujaa huwa mfalme. Baba yake shujaa Mukwavinyika alikuwa mfalme aliyetawala katika jamii ya Wahehe aitwaye Munyigumba. Mtawala huyu alikuwa mtu mwenye nguvu nyingi za kivita zilizomuwezesha kushinda vita na kuteka jamii za jirani. Suala hili limeelezwa pia na Mumford (1934) kuwa Muyigumba alikuwa na mtoto wake aliyejulikana kwa jina la Mukwavinyika ambaye naye aliteka na kuvamia vijiji vya jirani kama ambavyo alifanya baba yake. Siku moja Munyigumba alivamiwa na jeshi la Wangoni katika utawala wake. Hata hivyo, mfalme huyu alifanikiwa kuokolewa na mtoto wake aitwaye Mukwavinyika, wakati akiwa bado kijana mdogo. Suala hili linabainika wazi katika Kisakale cha Mukwavinyika kama ifuatavyo:

- 1) ...Siku moja jeshi la Wangoni lilipenya Ubena likaingia Uhehe ili kumvamia Munyigumba katika utawala wake. Wangoni hao, walikuwa wamechachamaa kama moto uliochochewa kuni kavu kutokana na bangi waliyozoea kuivuta kabla ya mapiganoo. Hivyo, hawakuwa na hofu wala kujali maumivu, jeraha au kifo kama mawimbi ya mafuriko yasiyoweza kuzuiwa. Kwa sababu hiyo, Munyigumba hakuweza kuwapiga Wangoni akawa hana budi kukimbilia kwenye mapango ya Nyamulenge. Hata hivyo, Wangoni walimtafuta na kujua kuwa Munyigumba alijificha pangoni, wakamfuata na kumziba mle pangoni ili asiweze kutoka. Kwa bahati nzuri, huko nyuma, vikosi vya Munyigumba vilivyokuwa vinaongozwa na mtoto wake aitwaye Mukwavinyika, vilirejea. Mukwavinyika alikusanya vikosi vyake haraka na akachukua dawa ya kiutawala iliyoitwa “lihomelo” akafanya kama ambavyo alielekezwa na baba yake. Ghafla, walipokuwa pangoni Munyigumba akashangaa kuona dawa aliyokuwa nayo inaanza kufuka moshi na inageuka rangi na kuwa nyekundu. Kitendo cha dawa kugeuka rangi ilikuwa ishara kwamba watakombolewa...

Maelezo katika Data Na. 1 hapo juu yanathibitisha kuwa baba mzazi wa shujaa Mukwavinyika alikuwa mfalme aliyetawala katika jamii ya Wahehe. Suala la baba mzazi wa shujaa kuwa mfalme limejitokeza pia kwa mashujaa wengine wa Kiafrika (taz. Okpewho, 1979; Mulokozi, 1999 na Mahenge, 2016). Akifafanua suala hilo, Okpewho (1979) anaeleza kwamba shujaa ni mtu anayetoka katika tabaka la juu kama ilivyo kwa Mwindo na Kambili amba walikuwa mashujaa waliotoka katika tabaka la juu kwa sababu baba zao walikuwa wafalme. Naye Mulokozi (1999) anaeleza kuwa shujaa hutoka katika tabaka la juu kama ilivyo kwa Rukiza ambaye baba yake alikuwa mtawala wa mji wa Kiziba. Vilevile, Mahenge (2016) anaeleza kuwa shujaa Lwembe anatoka katika tabaka la juu kwa sababu baba yake alikuwa mtawala katika jamii ya Wakinga. Hii ni ithibati kuwa mara nyingi shujaa wa Kiafrika huwa mtoto wa mfalme au mtawala wa jamii fulani kama ilivyojibainisha kwa mashujaa mbalimbali wa Kiafrika, akiwamo Mukwavinyika.

4.2 Kuzaliwa kwa Shujaa ni kwa Kawaida

Hatua nyingine inayojibainisha katika makuzi ya shujaa Mukwavinyika ni kuzaliwa kawaida. Kwa mfano, Ngassapa (2011) anaeleza kuwa Mukwavinyika alizaliwa mwaka 1855 katika kijiji cha Luhota kilichopo mkoani Iringa. Halikadhalika, hakuna taarifa zozote zinazosimulia kuhusu maisha ya Mukwavinyika alipokuwa mtoto mdogo, zaidi ya kuambiwa jina lake alilopewa na wazazi wake baada ya kuzaliwa. Inasemekana kuwa Mukwavinyika alipozaliwa aliitwa *Ndasalasi* jina lenye maana ya ‘apapasaye kwa mikono na vidole akitafuta kitu’. Suala hili pia linasimuliwa na mtoataarifa wetu kutoka Kalenga:

- 2) ...Mukwavinyika alizaliwa Luhota mwaka wa 1855. Kuhusu utoto wake hakuna habari zozote maalumu isipokuwa kwamba aliitwa kwa jina la *Ndasalasi* likiwa na maana ya ‘apapasaye kwa mikono na vidole atafutapo kitu...’

Maelezo katika Data Na. 2 yanathibitisha kuwa kuzaliwa kwa shujaa Mukwavinyika kulikuwa kwa kawaida kwa sababu hakuna masuala yoyote ya kimiujiza au kimazingara yaliyojitekeza katika utungaji mimba mpaka kuzaliwa kwake. Hapa inabainika tofauti na alivyoeleza Raglan (1934) kuwa, mazingira ya kutungwa mimba na ya kuzaliwa kwa shujaa huwa ya kimazingara ambapo inasemekana huwa mwana wa Mungu. Suala la shujaa kuhusishwa na uungu linafafanuliwa pia na Knappert (1983) anayesema kuwa mashujaa wa Ulaya na Asia kabla ya majilio ya Ukristo na Uislamu wana nduni ya uungu ndani yake. Akifafanua hoja hiyo, Gathara (2015) anaeleza kuwa katika mashujaa wa kidini huwa kuna utabiri wa kuzaliwa kwa shujaa uliofanyika miaka ya zamani. Kwa mfano, kuzaliwa kwa Yesu (Isa) kulibashiriwa katika Agano la Kale katika Isaya 7:14 na kunathibitishwa na Yohana (Yahya) Mtakatifu. Utabiri wa Yesu (Isa) ulitimia katika kitabu cha Mathayo 2:1 ambamo mnaelezwa kuwa shujaa alizaliwa Bethlehemu ya Uyahudi, zamani za mfalme Herode. Hata hivyo, hali hii ni tofauti na kwa mashujaa wa kijadi. Kwa mfano, Sungi (2011) aligundua kuwa kuzaliwa kwa mashujaa katika jamii ya Wanyanyembe wa Tabora kulikuwa kwa kawaida. Hii ina maana kwamba kuzaliwa kwa shujaa wa kijadi hakufungamani na maajabu au utabiri wa aina yoyote ile kama inavyojibainisha kwa mashujaa wa kidini. Kwa upande wa mashujaa wa kidini, walio wengi, kuzaliwa kwao kunafungamana na utabiri, mambo ya ajabuajabu yanayohusiana na mazingara. Suala hili linaonesha utofauti uliopo kati ya shujaa wa kijadi na shujaa wa kidini aliye na sifa za uungu ndani yake.

4.3 Shujaa Alifanyiwa Jaribio la kutaka Kuuawa na Mpinzani wake

Mbali na hatua hizo, pia Mukwavinyika alipokuwa kijana alifanyiwa jaribio la kutaka kuuawa na mpinzani wake aitwaye Mwambambe. Hoja hii pia imefafanuliwa na Raglan (1934) kuwa shujaa anapozaliwa huwa linafanywa jaribio, aghalabu na baba yake mzazi, la kutaka kumuua. Maelezo yaliyotolewa na Raglan

(1934) hayatofautiana na jambo lililojitokeza kwa Mukwavinyika ambaye mpinzani wake aitwaye Mwambambe alitaka kumuua. Mwambambe alikuwa mtu katili na aliyekuwa akiua watu ovyoovyo. Ikumbukwe kuwa, Mwambambe hakuwa mtawala wa Uhehe bali alipata madaraka kwa nguvu baada ya kumpindua Mukwavinyika. Nukuu katika Data Na. 3 inayofuata inathibitisha hoja ya shujaa kufanyiwa jaribio la kuuawa katika Kisakale cha Mukwavinyika.

- 3) ...Wahehe wengi walikuwa wanamuogopa Mwambambe na waligeuza hofu yao kuwa chuki kubwa. Katika utawala wake, Mwambambe alikuwa anaua watu ovyoovyo kama anachinja kuku. Hata Mukwavinyika mwenyewe alikuwa kwenye orodha ya watu ambaao alipanga kuwaua...

Suala lililo wazi hapa ni kwamba mashujaa wengi wa Kiafrika wanakutana na misukosuko ya kutaka kuuawa na maadui zao, hasa kwa ajili ya kugombania madaraka. Kwa mfano, Mtega (2017) anamuelezea mtawala Mkami kuwa alipata mtoto wa kiume lakini kutokana na hofu ya utawala wake alimfanyia sihiri ili atupwe na asiweze kurithi utawala wake. Hivyo, Mkami alitupwa katika maji na baba yake mzazi akitegemea kuwa atauawa na wanyama wakali ili asije akatawala katika ardhi ya baba yake.

4.4 Shujaa Anasafiri kwa Kutoroshwa kwa Siri

Mukwavinyika katika makuzi yake amepitia hatua ya kusafiri kwa kutoroshwa kwa siri. Kwa mfano, Senkoro (1997) amebainisha sifa kuu ya mashujaa katika ngano za Zanzibar kuwa ni safari. Hivyo, Senkoro anaeleza kuwa shujaa ni lazima asafiri kutoka nyumbani kwenda kuishi mahali pengine. Hapa inabainika kuwa lazima shujaa aondoke nyumbani na kwenda kuishi sehemu nyingine kisha anarudi tena kuishi nyumbani. Katika Kisakale cha Mukwavinyika, imebainika kuwa Mukwavinyika alitoroka kwa siri kutoka nchi ya Uhehe na kwenda kuishi nchi ya Ugogo. Suala hili la shujaa kutoroshwa kwa siri limebainishwa pia na Raglan (1934). Mukwavinyika alitoroka kwa siri kwa sababu alikuwa anaogopa kuuawa na mpinzani wake, Mwambambe. Ikumbukwe kuwa baada ya baba yake mzazi Mukwavinyika kufariki dunia, utawala wa nchi ya Uhehe ulikabidhiwa kwa mtoto wake Mukwavinyika. Hata hivyo, kitendo cha Mukwavinyika kuachiwa madaraka hakikumpendeza Mwambambe aliyeamua kufanya mapinduzi dhidi ya Mukwavinyika. Baada ya mapinduzi kufanyika na Mwambambe kuchukua utawala, njama za kutaka kumuua Mukwavinyika zilifanywa. Kutokana na hayo Mukwavinyika aliona bora kutoroka ili kukwepa kifo. Katika kisakale hicho imeelezwa kama ifuatavyo:

- 4) ...Mukwavinyika alipokuwa anatoroka alijipaka udongo mwekundu usoni kisha akajifunika nguo mwili mzima na akapita

katika nchi ya Uhehe bila kugundulika akaelekea katika nchi ya Ugogo...

Maeleo katika Data Na. 4 yanathibitisha kuwa Mukwavinyika alitoroka kwa siri kutoka nchi ya Uhehe na kwenda kuishi nchi ya Ugogo akikimbia kifo. Hivyo, imebainika kuwa shujaa lazima asafiri kwa sababu maalumu. Kwa mfano, Kemunto (2015) anazitaja sababu kadhaa zinazoweza kumsababisha shujaa kusafiri na kwenda kuishi sehemu nyingine kuwa ni pamoja na kutafuta utambulisho wa jamii yake, kutafuta nchi nzuri, kutafuta mbinu za kulipiza kisasi, kutafuta mpenzi na kutafuta mbinu za kuiokoa jamii yake. Naye Sosoo (2018) anasema kwamba shujaa wa Kiafrika husafiri kwenda kuishi katika nchi ya mbali kwa sababu maalumu. Hivyo, jambo lililomsababisha Mukwavinyika kusafiri kwenda kuishi Ugogoni ni kukimbia kifo.

4.5 Shujaa Analelewa na Ndugu yake katika Nchi ya Mbali

Mbali na hatua hizo, hatua nyingine katika makuzi ya shujaa aliyoipitia Mukwavinyika ni kulelewa na ndugu yake katika nchi ya mbali. Kama alivyobainisha Raglan (1934) kuwa mara nyingi shujaa analelewa na wazazi wa kambo katika nchi ya mbali. Hili ni suala linalojibainisha pia kwa shujaa Mukwavinyika aliyelelewa na ndugu yake katika nchi ya Ugogo baada ya kumkimbia Mwambambe (taz. Data Na. 4). Baada ya kufika Ugogoni, Mukwavinyika alilelewa na baba yake mdogo aliyeitwa Muyovela. Suala hili limebainika katika kisakale hicho kama ifuatavyo:

- 5) ...Baada ya Mwambambe kufanya mapinduzi ya kumpindua Mukwavinyika, Mukwavinyika alikimbilia kwa baba yake mdogo aitwaye Muyovela aliyekuwa akiishi katika nchi ya Ugogo...

Kutokana na hayo yaliyoelezwa katika Data Na. 5, inathibitika kuwa Mukwavinyika alilelewa na ndugu yake katika nchi ya mbali. Suala hili la shujaa kulelewa na ndugu zake katika nchi ya mbali limejidhihirisha pia kwa mashujaa wengine wa Kiafrika. Kwa mfano, Sungi (2011) alifanya utafiti wa ruwaza ya shujaa mwanamke wa jamii ya Wanyanyembe wa Tabora na kueleza kuwa shujaa huondoka na kwenda kulelewa katika nchi za mbali akitafuta maisha.

4.6 Kurejea kwa Shujaa katika Ufalme wa Baba yake

Hatua nyingine inayojibainisha katika makuzi ya shujaa Mukwavinyika ni kurejea na kutawala katika ufalme wa baba yake kama asemavyo Raglan (1934) kuwa mara nyingi shujaa hurejea na kutawala katika ufalme wake wa baadaye. Baba mzazi wa Mukwavinyika alipofariki dunia aliacha wosia kuwa utawala wa jamii ya Wahehe utabaki chini ya mtoto wake aitwaye Mukwavinyika. Hata hivyo, Mukwavinyika alikabidhiwa madaraka katika kipindi hicho akiwa bado kijana mdogo. Kitendo hicho kilimuumiza sana Mwambambe aliyekuwa mfuasi na jemadari mwaminifu

wa baba yake Mukwavinyika. Baada ya kuisha kwa msiba wa baba yake Mukwavinyika, Mwambambe aliamua kufanya mapinduzi dhidi ya Mukwavinyika kisha akachukua nchi. Kutokana na hayo, Mukwavinyika aliamua kukimbia kwa kuogopa kifo na kwenda kuishi Ugogoni. Baada ya kuishi Ugogoni kwa muda mrefu hatimaye, Mukwavinyika alirejea katika nchi ya Uhehe. Mukwavinyika alirejea baada ya kuitwa na Wahehe waaminifu ambao hawakuridhika na utawala wa Mwambambe. Suala hili linaleezwa katika Kisakale cha Mukwavinyika kama ifuatavyo:

- 6) ...Utawala wa Mwambambe ulikuwa ni utawala wa kikatili kama wa Adolf Hitler. Wahehe hawakuridhika na utawala huu. Hivyo, Wahehe walifanya shauri kwa siri kisha wakatayarisha wanavita waaminifu na kumuita Mukwavinyika ili arudi kuwaongoza kumpiga vita Mwambambe...

Maelezo katika Data Na. 6 yanathibitisha kuwa Mukwavinyika alitawala rasmi katika utawala wa baba yake baada ya kumfukuza Mwambambe madarakani. Suala hili lilielezwa pia na watafiti wa mashujaa wa Kiafrika kuwa mara nyingi watoto wa mashujaa hutawala katika himaya za baba zao (taz. Mofolo, 1975 na Mtega, 2017). Akifafanua suala hilo, Mofolo (1975) anaeleza kwamba, shujaa Shaka Zulu alipewa sihiri kutoka kwa mganga, sihiri ambayo ilimsaidia kurithi utawala wa baba yake. Ikumbukwe kuwa, hapo awali Shaka alifukuzwa katika utawala wa baba yake; hata hivyo, Shaka alipambana na akafanikiwa kutawala katika ardhi ya baba yake. Si hivyo tu, pia Mtega (2017) anamwelezea mtoto wa Mkami kuwa, ingawa wazazi wake walimtupa katika mto, lakini baada ya mtoto huyo kuwa mkubwa, alirudi nyumbani na kutawala katika himaya ya baba yake.

4.7 Shujaa Anapata Ushindi dhidi ya Mfalme au Jitu

Watafiti wa masuala ya mashujaa wanaeleza kwamba mara nyingi shujaa hukumbana na vikwazo vya aina mbalimbali anapokuwa safarini. Halikadhalika, katika mapambano hayo shujaa hushinda na kudhihirisha ushujaa wake (taz. Raglan, 1934 na Campbell, 1949). Katika Kisakale cha Mukwavinyika imeelezwa kwamba Mukwavinyika alirejea kutawala tena katika ufalme wa baba yake baada ya kushinda vita dhidi ya Mwambambe. Ikumbukwe kuwa Mwambambe lilikuwa jitu lenye nguvu na la kutisha. Hivyo, Mukwavinyika alipata wakati mgumu kumuua Mwambambe kwa sababu Mwambambe alikuwa amejizindika kwa dawa za kienyeji. Kutokana na kinga aliyojizindika, Mwambambe hakudhurika kwa kitu chochote akiwa vitani mpaka pale siri ya zindiko lake ilipojulikana. Kila alipochomwa mkuki aliuchomoa na kuwachoma maadui zake bila ye ye mwenyewe kudhurika wala kufa. Katika hali ya kawaida, haiwezekani mwanadamu achomwe mkuki asife au kudhurika. Hivyo, kinachoelezwa kuhusu Mwambambe hapa ni mizungu iliyofungamana na sihiri. Kutokana na hayo, msaada wa kumuua

Mwambambe uliletwa na baba mzazi wa Mukwavinyika. Suala hilo limeelezwa katika kisakale hicho kama ilivyonukuliwa katika Data Na. 7 ifuatayo:

- 7) ...Munyigumba alimweleza Mukwavinyika mbinu za kumuua Mwambambe. Alimweleza kuwa “ili Mwambambe afe, anatakiwa achomwe mkuki katika dole gumba au kwenye kisigino.” Baada ya kuijua mbinu hiyo, Mukwavinyika alimwambia Mkimayena amchome mkuki Mwambambe kama ilivyoelekezwa. Mkimayena alimchoma mkuki Mwambambe kwenye dole gumba na kwenye kisigino na hapohapo Mwambambe alianza kuhisi kichefuchefu. Hata hivyo, inaonekana mkuki huo haukumwingia vizuri. Askari mwingine wa Mukwavinyika aitwaye Mwakapanzi alitupa mkuki ambaao ulimpata Mwambambe mpaka ukatokeza upande wa mgongo. Watu walioshuhudia walimuona Mwambambe anaishiwa nguvu na kuanguka chini puuuuuuuuu! kama gunia. Basi baada ya Mwambambe kukata roho, majeshi ya Mukwavinyika yalikula maiti ya Mwambambe kisha wakailamba damu iliyokuwapo kwenye mchanga huku wakiwa na imani kuwa nguvu alizokuanazo Mwambambe zitawaingia wao...

Data Na. 7 hapo juu inabitisha jinsi shujaa Mukwavinyika alivyopata ushindi baada ya kufanikiwa kumuua Mwambambe. Ushindi huo aliupata baada ya kusaidiwa na baba yake mzazi aliymweleza mbinu za kumuua Mwambambe. Hivyo, shujaa hupata msaada katika kupambana na masaibu ya aina mbalimbali kama asemavyo Senkoro (1997) kuwa, shujaa akiwa safarini hupambana mwenyewe na mara nyingine huweza kupata msaada kutoka kwa ndege, mtu, wazazi au kitu chochote. Si hivyo tu, pia Sikuomba (2018) anatoa mfano wa ujasiri na uhodari wa shujaa Kanyamaishwa alivyopambana na kufanikiwa kumuua chui kama ambavyo Shaka alipambana kumuua simba katika jamii ya Wazulu.

4.8 Shujaa Anakuwa Mfalme

Mbali na hatua hizo za makuzi zilizoelezwa, Mukwavinyika pia alikuwa mfalme. Raglan (1934) anaeleza kuwa mara nyingi shujaa anakuwa mfalme anaposhinda katika mapambano dhidi ya vikwazo vyta aina mbalimbali. Tukirejea kwa shujaa Mukwavinyika, alipata ufalme baada ya kumshinda Mwambambe vitani. Katika mapigano makali sana ya kivita, Mwambambe aliamua kuikimbilia nchi ya Uhehe na kwenda kuishi katika nchi ya Ukimbu. Suala hili limeelezwa katika Kisakale cha Mukwavinyika kama ilivyonukuliwa katika Data Na. 8.

- 8) ...Mukwavinyika aliporudi Uheheni hakukawia kusimamisha jeshi la Wahehe waaminifu kisha akamshambulia Mwambambe pande zote na kumsukuma mbele mpaka Usawila. Katika mapigano makali sana, Mwambambe akashindwa na akawa hana budi zaidi ya kukimbilia nchi nyingine. Mwambambe alichagua kukimbilia Kiwere katika nchi ya Ukimbu...

Maelezo katika Data Na. 8 yanabainisha kuwa Mukwavinyika alitawala na kuwa mfalme baada ya kufanikiwa kumfukuza Mwambambe madarakani. Hoja hii pia imefafanuliwa na mtoa taarifa wetu wa uwandani:

- 9) ...Mwambambe pamoja na wafuasi wake waliuliwa na jeshi la Mukwavinyika huko Ilundamatwe. Kutokana na ushindi alioupata Mukwavinyika dhidi ya Mwambambe, Mukwavinyika alitawazwa rasmi kuwa Mtawala wa Wahehe...

Hivyo basi, mara baada ya Mukwavinyika kumshinda Mwambambe, Mukwavinyika alitawala rasmi katika nchi ya Uhehe alioachiwa na baba yake. Suala hili linashahibiana na mashujaa wa jamii zingine za Kiafrika. Kwa mfano, Mtega (2017) anaeleza kuwa Kanyamaishwa baada ya kupambana katika vita, hatimaye alifanikiwa na akatawala katika ardhi ya baba yake.

4.9 Shujaa Anatawala bila Mkasa na Kutunga Sheria

Hatua nyininge alioipitia shujaa Mukwavinyika katika makuzi yake ni kutawala bila mkasa na kutunga sheria. Mara baada ya kuchukua madaraka kutoka kwa Mwambambe, Mukwavinyika alitawala Uheheni bila matatizo yoyote kwa sababu Wahehe wengi walikuwa wanampenda. Utawala wowote ule katika jamii yoyote huongozwa na kuwapo kwa sheria na kanuni mbalimbali. Mukwavinyika alipokuwa mfalme alitunga sheria mbalimbali alizozitumia kuongoza wananchi wake kama asemavyo Raglan (1934) kuwa shujaa kwa muda fulani anatawala bila mkasa na kutunga sheria. Kwa mfano, Wright (1961) anafafanua baadhi ya sheria alizozitumia Mukwavinyika kuwa alikuwa mtawala aliyetoza ushuru wa lazima misafara ya kibashara iliyokuwa inapita katika eneo lake. Aidha, anaeleza kuwa Mukwavinyika alikuwa mtawala mwenye nguvu kwa kipindi hicho. Hivyo, watu wote waliokataa kulipa kodi alikuwa anawakamata na kuwateka. Anaeleza kuwa kitendo hiki cha Mukwavinyika kulipisha kodi kilikuwa kikwazo kikubwa kwa Wajerumani amba walikuwa wameshaingia Tanganyika. Suala hilo limeelezwa katika kisakale hicho katika Data Na. 10 kama ifuatavyo:

- 10) ...Wajerumani walikuwa wanamwogopa Mukwavinyika kwa sababu walijua ni mfalme mwenye nguvu katika mambo ya kivita ambaye angeweza kuwapinga. Hivyo, Wajerumani walijenga ngome zao Mpwapwa, Kilosa na Kilimatinde ili kujilinda naye. Hata hivyo, wenyeji wa sehemu hizo bado walikuwa wanamlipa kodi Mukwavinyika kwa jinsi walivyokuwa wanamwogopa...

Suala la shujaa Mukwavinyika kuunda sheria zilizomsaidia kutawala katika kipindi cha utawala wake lilielezwa pia na mtoataarifa wetu wa uwandani kama ifuatavyo:

- 11) ...Kila mwananchi alikuwa analipa kodi ya mapato kwa Mutwa Mukwavinyika isipokuwa askari, watoto na wazee. Pia, Mutwa Mukwavinyika aliunda jeshi ambalo lilikuwa na vikosi sita vyenye majukumu mbalimbali katika suala zima la kulinda usalama. Kwa

wale askari waoga Mukwavinyika aliunda sheria kuwa kama utafanikiwa kuua adui unatakiwa umkate sehemu zake za siri na kisha kuchomeka katika mkuki mdogo ili baada ya vita unakwenda kumuonesha ajue kama kweli umeua adui...

Yaliyoelezwa katika Data Na. 11 yanathibitisha kuwa Mukwavinyika aliunda baadhi ya sheria na kanuni zilizomsaidia kuongoza nchi. Miongoni mwa sheria hizo ni kila mwananchi kutakiwa kulipa kodi kwa ajili ya kufanya maendeleo katika jamii.

4.10 Shujaa Anasalitiwa na Raia wake

Mukwavinyika kusalitiwa na raia wake ni hatua nyingine ya makuzi aliyoipitia ambayo ilijibainisha katika kisakale kinachomhusu. Katika kisakale hicho imeelezwa kuwa Mukwavinyika alisalitiwa na jamaa zake wa karibu ambao ni Mbogamasoli na Msatima. Mukwavinyika alisalitiwa na ndugu zake hao wakati wa mapambano dhidi ya Wajerumani. Suala hili limeelezwa kama ilivyonukuliwa katika Data Na. (12).

12) ...Mbogamasoli alitaka yeye ndiyo awe kiongozi katika kikosi hicho cha kivita. Mbogamasoli alipoona hakuna anayejali alimsaliti Mukwavinyika kwa maadui wa Kijerumani ambao waliwashambulia katika vita ya awamu ya pili. Hata hivyo baada ya kufanya usaliti huo, Mbogamasoli alikuja kujulikana na kuuliwa kwa amri ya Mukwavinyika...

Hapa inabainika kuwa shujaa Mukwavinyika alisalitiwa na ndugu yake wa karibu aitwaye Mbogamasoli. Sababu kuu iliyomfanya Mbogamasoli kumsaliti Mukwavinyika kwa Wajerumani ni uchu wa madaraka. Raglan (1934) anaeleza kuwa mara nyingi shujaa hukataliwa na miungu au na raia wake. Suala la shujaa kukataliwa na raia wake limejitokeza pia kwa mashujaa wengine wa Kiafrika. Kwa mfano, Gathara (2015) anaeleza kuwa shujaa Yesu (Nabii Isa) alipangwiwa njama ya kuuawa na baadaye aliteswa na kusulubiwa msalabani na wale waliodai kuwa hakuwa Yesu (Nabii Isa) mwenyewe, na kisha akauawa. Kwa mujibu wa Bibilia, Wayahudi walifanikiwa kumsulibisha na kumuua Yesu (Nabii Isa). Naye Sosoo (2018) anasema kuwa mara nyingi mashujaa wa Kiafrika hukataliwa kwa kusalitiwa na watu wao wa karibu kama ilivyoolezwa na Raglan (1934). Watu hao wanaomsaliti shujaa wanawenza kuwa watoto wa shujaa au ndugu zake wa karibu. Aidha, Lyamuya (2014) anaeleza kwamba usaliti kwa shujaa mara nyingi hufanywa na mtu wa karibu yake. Mtu huyo anaweza kuwa mtoto wa shujaa, mke wa shujaa, dada au kaka wa shujaa. Pia, Lyamuya anaendelea kueleza kuwa kuna sababu kwa nini shujaa anasalitiwa; yawenza kuwa kwa sababu ya uchu wa madaraka, tamaa ya mali au tamaa ya mapenzi. Mashujaa wa Kiafrika, baada ya kusalitiwa, mara nyingi hukamatwa na kuuawa kirahisi na maadui zao.

4.11 Shujaa Anaondolewa katika Kiti chake cha Enzi

Hatua nyingine aliyoipitia shujaa Mukwavinyika katika makuzi yake ni kuondolewa katika kiti chake cha enzi. Watafiti wa masuala ya ruwaza ya shujaa wanaeleza kuwa shujaa huwa anaondolewa katika kiti chake cha enzi na kufukuzwa mijini kinguvu (taz. Raglan, 1934). Kwa upande wa Mukwavinyika, Wright (1961) anafafanua kuwa baada ya miaka kadhaa kupita, Mukwavinyika alijenga ngome kubwa huko Kalenga. Hata hivyo, Wajerumani, kwa kuwa walikuwa na uadui na Mukwavinyika, walienda kuivamia ngome hiyo. Walipofika Kalenga, Mukwavinyika alifanikiwa kutoroka na akaendesha vita vya msituni. Alipokuwa msituni, Mukwavinyika alisaidiwa na Wahehe kwa kupelekewa chakula na walishirikiana naye katika vita hivyo na kuvifanya kuwa vita vigumu kwa Wajerumani. Suala hili limebainika katika kisakale hicho kama ifuatavyo:

- 13) ...Hata alipokuwa huko msituni, Wahehe walikuwa wanapika chakula na kuweka hovyo msituni ili Mukwavinyika akipita ale na asife na njaa. Hata wakati mwininge askari wa Kijerumani walipokuwa karibu kumkamata, Wahehe walijitupa ovyo mbele yao wasijali maumivu au kifo ili mradi Mutwa wao apate kujificha...

Maelezo katika Data Na. (13) yanaonesha jinsi Mukwavinyika alivyopigana vita vya msituni huku akisaidiwa na Wahehe ambao hawakuogopa chochote bali waliambatana na mtawala wao katika mapigano ya kivita. Hii inaonesha kuwa shujaa Mukwavinyika alihama kutoka Kalenga na kwenda kuishi msituni kwa sababu alikuwa anaogopa kukamatwa na Wajerumani.

4.12 Shujaa Anajiua kwa Kujiipa Risasi

Mbali na hatua zilizobainishwa awali, hatua inayofuata aliyoipitia shujaa Mukwavinyika katika makuzi yake ni kujiua kwa kujiipa risasi. Mukwavinyika hakuogopa kifo na aliona heri kufa kuliko kukamatwa na Wajerumani. Baada ya kuona anakaribia kukamatwa na Wajerumani, Mukwavinyika alijiua mwenyewe kwa kujiipa risasi, na hivyo, kujiumbia hatima yake badala ya hatima hiyo kuumbwa na Mungu. Suala hili, limeelezwa katika kisakale hicho kama ilivyonukuliwa katika Data Na. (14).

- 14) ...Mukwavinyika alipokuwa huko Mulambalasi aliona Mwasamila amewahi kurudi na kishaijua siri yake kuwa anataka kujiua alianza kwanza kummiminia risasi Mwasamila kama mvua na kisha akajiua na yeye mwenyewe puuuuuu!

Maelezo katika Data Na. 14 ni ithibati kwamba Shujaa wa Kiafrika haogopi kifo. Anaona heri kufa kuliko kupata fedheha baada ya kukamatwa na maadui. Ikumbukwe kuwa mashujaa wa Kiafrika ni viongozi na watetezi wa wanajamii, hivyo basi, ili kulinda heshima ya shujaa, shujaa hupambana na maadui zake mpaka dakika ya mwisho. Gathara (2015) anaeleza kuwa mashujaa wa Kiafrika huamua kufa kikondoo au kuhatarisha maisha yao kwa sababu kifo ni muhimu kuliko

maisha. Anaendelea kufafanua kuwa kifo cha shujaa ni wokovu kwa jamii nzima kwa kuwa kimepangwa na Mungu. Suala hili limebainishwa pia na Raglan (1934) aliposema kuwa shujaa anakufa kimazingara. Hii inamaanisha kwamba shujaa hafi hivihivi tu, bali vifo nya mashujaa huwa nya ajabuajabu.

4.13 Shujaa Anakufa Juu ya Kilima

Raglan (1934) anaeleza kwamba mara nyingi shujaa hufariki juu ya kilima. Hali ni hiyohiyo hata kwa shujaa Mukwavinyika ambaye alifariki katika mlima Mulambalasi. Willoughby na wenzake (2019) wanaeleza kwamba, baada ya Mukwavinyika kufariki dunia, mwili wake ulizikwa katika eneo la umbali mfupi kutoka katika mlima mkubwa uitwao Mulambalasi. Katika eneo hilo, mwaka 1998, serikali ilijenga mnara wa kumbukumbu wa kuadhimisha miaka mia moja ya kifo cha Mukwavinyika.

Katika Kisakale cha Mukwavinyika imebainika kuwa Mukwavinyika alisafiri kwa mara ya pili kutoka Kalenga na kwenda kuishi katika mlima Mulambalasi. Kama ilivyokuwa kwa safari ya awali, katika safari hii pia shujaa Mukwavinyika alikuwa anakimbia hatari ya kukamatwa na Wajerumani ambao alikuwa na vita nao. Hata hivyo, tofauti na safari ya kwanza ambapo alirejea, katika safari hii ya pili hakurejea, bali alikufa kwa kujipiga risasi (taz. Data Na. 14). Hivyo, hapa imebainika kuwa Shujaa Mukwavinyika alipoona anaishiwa nguvu katika mapigano ya kivita dhidi ya Wajerumani alikimbilia msituni katika mlima Mulambalasi. Hata alipokuwa huko mlimani, alipoona anakaribia kukamatwa na Wajerumani aliamua kuijua kwa kujipiga risasi ili asikamatwe na Wajerumani. Hivyo, Mukwavinyika alifariki katika mlima Mulambalasi kwa kujipiga risasi.

4.14 Mtoto wa Shujaa Anarithi Utawala wa Baba yake

Mbali na hatua hizo, hatua nyingine katika ruwaza ya shujaa Mukwavinyika imebainika kuwa mtoto wa shujaa alirithi utawala baada ya baba yake mzazi kufariki dunia. Mara baada ya shujaa Mukwavinyika kufariki dunia kwa kujipiga risasi, utawala wa nchi ya Uhehe ulikabidhiwa mikononi mwa mtoto wake wa kwanza wa kiume Sapi. Suala hili linathibitisha kuwa utawala katika jamii za Kiafrika ni wa kurithishana, kutoka kwa baba Kwenda kwa mtoto wa kiume. Suala hili limejitokeza tofauti na Raglan (1934) aliposema kuwa watoto wa shujaa, kama wapo, huwa hawarithi utawala wa baba zao. Hali hii ni tofauti, katika kisakale cha Mukwavinyika kwa sababu utawala wake ulikabidhiwa kwa mtoto wake. Suala hili limeelezwa na mmoja wa watoataarifa za uwandani:

- 15) ...Sapi aliongoza nchi baada ya baba yake kufariki dunia...ingawa naye hakutawala kwa muda mrefu kwa sababu Wajerumani walimchukua na wakampeleka kusoma huko kwao Ujerumani...

Maelezo katika Data Na. 15 yanathibitisha kuwa mtoto wa Mukwavinyika aitwaye Sapi ndiye aliyerithi utawala wa baba yake. Suala hili pia linaelezwa na Ngassapa

(2011) alipotaja watawala waliotawala Uheheni kuwa kuna Mwamuyinga, Kilonge, Munyigumba, Mwambambe, Mukwavinyika, Sapi na Adam Sapi. Suala hili linaelezwa pia na watafiti wa mashujaa wa Kiafrika kuwa mara nyingi watoto wa mashujaa hutawala katika himaya za baba zao (taz. Mofolo, 1975 na Mtega, 2017).

4.15 Shujaa Anakuwa na Madhabahu Moja au Zaidi za Matambiko yake

Katika jamii za Kiafrika watu waliofariki dunia karibuni au zamani hukumbukwa kwa njia za kufanya matambiko (taz. Mbiti, 1969). Wahenga au mahoka hukumbukwa kwa kutajwa majina katika tambizi, kuombwa msaada wa mambo mbalimbali kama vile uzazi na kuondoa ukame pale inapobidi. Hivyo basi, njia hii hutumika kuwakumbuka mashujaa wa Kiafrika walipambana kuzikomboa jamii zao katika matatizo mbalimbali. Kwa mfano, shujaa Mukwavinyika wa jamii ya Wahehe anakumbukwa na wanajamii kwa njia ya sherehe na matambiko. Sherehe hizo na matambiko hayo mara nyingi hufanyika katika kijiji cha Kalenga ambapo limehifadhiwa fuvu la shujaa Mukwavinyika. Kwa mfano, Glickman (1969) anaeleza kuwa jamii ya Wahehe inakumbukwa sana na Wajerumani kwa sababu Wajerumani walichukua fuvu la kichwa cha Mukwavinyika na kukihifadhi katika makumbusho ya Bremen, Ujerumani. Hata hivyo, ilipofika mwaka 1954, fuvu hilo la Mukwavinyika lilitudishwa nchini Tanzania na kuhifadhiwa katika Makumbusho ya Kalenga. Kuhusu kufanya matambiko ya ibada, Malangalila (1987) anatoa mfano wa imani katika *misoka* ambapo anaeleza kuwa wakati wa masika, pale inapotokea mvua imechelewa kunyesha, Wahehe huenda katika makaburi ya ndugu zao na kuchinja ng'ombe dume mweusi, kondoo mweusi pamoja na kuweka pombe. Baada ya kufanya hivyo, mvua hunyesha huku ikifuatana na radi na umeme. Suala hili limefafanuliwa pia na mmoja wa watoataarifa wetu wa uwandani anapoeleza:

- 16) ...Mara nyingi kama tukikosa mvua katika kijiji chetu huwa tunaenda kwenye kaburi la Mukwavinyika lililopo Mulambalasi, tunamuomba atusaidie kupata mvua. Tulichukua kondooo na tukaenda kumchinja juu ya kaburi la Mukwavinyika huku tukiwa tunasema shida yetu. Wee bwana weee baada ya kumaliza kufanya hivyo ilinyesha mvua kubwa sana watu walifurahi na kushangilia kwa sababu Mukwavinyika alijibu maombi yetu...

Maelezo katika Data Na. 15 yanaonesha kuwa Mukwavinyika ana sehemu za matambiko yake zilizopo huko Kalenga na mlima Mulambalasi. Hii ni ithibati kuwa mashujaa wanakumbukwa na wanajamii kwa njia za kufanya matambiko. Matambiko yanafanyika sana katika jamii za Kiafrika kwa sababu watu waliwaachia wahenga suluhisho la matatizo yao (taz. Mbiti, 1969).

5.0 Kufanana na Kutofautiana kwa Vipengele katika Ruwaza za Mashujaa

Kutokana na tuliyoyajadili katika uchambuzi wa data, imebainika kuwa kuna vipengele vilivyojitokeza katika ruwaza ya shujaa kwa mujibu wa Raglan (1934) pia vimejitokeza katika ruwaza ya shujaa Mukwavinyika. Kama asemavyo Mulokozi (2017) kuwa kitendo cha vipengele katika ruwaza za mashujaa kufanana

kinatupatia muundo wa msingi wa ruwaza hizo na wenyе kutabirika. Hii ni ithibati kuwa jamii zina mfanano wa hapa na pale unaosababisha hata vipengele katika ruwaza za mashujaa ulimwenguni kufanana. Hata hivyo, kuna vipengele vinavyotofautiana. Suala hili ndilo linaloturudisha katika swali letu kuwa kama jamii zinatofautiana, tunawezaje kuwa na ruwaza ya shujaa inayofanana katika kila hali? Kutokana na uchambuzi wetu, imebainika kuwa vipengele katika ruwaza za mashujaa miongoni mwa jamii mbalimbali ulimwenguni, zaidi ya mfanano wa hapa na pale, vina tofauti za msingi na hivyo si sahihi kuvichukulia kuwa vya kimajumui.

Aidha, tumebaini sababu zinazosababisha vipengele vya ruwaza ya shujaa kutofautiana kama vile sifa ya uungu ikiwa na maana kwamba, mashujaa wa Ulaya na Asia walikuwa na sifa za uungu ndani yake tofauti na mashujaa wa kijadi wa Kiafrika ambao hawakuwa na sifa ya uungu. Christou (2001) anaeleza zaidi kuwa mashujaa wa Ugiriki, Italia, na India, mbali na kutumia sihiri, pia walikuwa makuhani wanaopeleka taarifa kwa miungu. Hoja hii ya Christou kwa namna moja ama nyingine inatufafanulia kuwa mashujaa ni watu wenyе nduni za uungu ndani yake.

Pia, mashujaa walionasibishwa na uungu ndani yao, utungaji wa mimba zao ulikuwa wa kimazingira na hata kuzaliwa kwa kulikuwa kwa ajabuajabu tofauti na mashujaa wasionasibishwa na masuala ya uungu ndani yake. Pia, kifo si mwisho wa uhai kwa Waafrika ikiwa na maana kwamba mashujaa wa Kiafrika hawakuogopa kifo ndio maana walijitoa mhanga kufariki kwa ajili ya jamii zao. Suala hili limesababisha hata miili yao kuzikwa na kuwa na sehemu za matambiko tofauti na alivyobainisha Raglan (1934) kuwa mwili wa shujaa hauzikwi. Vilevile, utaratibu wa kurithisha utawala kwa Waafrika kutoka kwa baba kwenda kwa mtoto wa kiume, umesababisha hata watoto wa mashujaa kuweza kurithi tawala za baba zao. Tofauti na Raglan (1934) aliposema kuwa watoto wa shujaa kama wapo huwa hawarithi tawala za baba zao.

6.0 Hitimisho

Makala haya yamechunguza ujitekezaji wa ruwaza ya shujaa wa Kiafrika katika Kisakale cha Mukwavinyika. Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa kwa mujibu wa Raglan (1934) ndiyo imeongoza uchambuzi wa data za makala haya. Kutokana na data zilizowasilishwa, imebainika kuwa shujaa Mukwavinyika amepitia hatua 15 katika makuzi yake kama zinavyojibainisha katika kisakale chake. Hivyo, ruwaza za mashujaa zilizopendekezwa na watafiti mbalimbali ulimwenguni ni mahali pa kuanzia katika kuchambua ruwaza za mashujaa wa Kiafrika. Kutokana na hilo, tafiti zaidi zinahitajika kwa mashujaa mbalimbali wa Kiafrika ili kubaini ruwaza zao zitakazotupa mwelekeo wa kauli jumuishi hasa kuhusu umbile la ruwaza ya shujaa wa Kiafrika.

Marejeleo

- Bowra, C. M. (1952) *Heroic Poetry*. London: Macmillan Publication.
- Campbell, J. (1949) *The Hero with a Thousand Faces*. California: New World Library.
- Christou, P. (2001) *Gods and Heroes in Greek Mythology: The Trojan War and the Odyssey*. London: Casa Editrice Bonechi Publisher.
- Finnegan, R. (1970) *Oral Literature in Africa*. Clarendon: Oxford University Press.
- Gathara, F. (2015) *Taswira ya Jagina katika Utendi: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Nabii Isa*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.
- Glickman, H. (1969) “Traditional Pluralism and Democratic Processes in Mainland Tanzania”. *Asian and African Studies*, Juz. Na. 5(1): 165-201.
- Hook, S. (1991) *The Hero in History: A Study in Limitation and Possibility*. London: Routledge Publisher.
- Johnson, J. (1978) *The Epic of Sunjata: An Attempt to Define the Model for African Epic Poetry*. Bloomington: Indiana University.
- Kemunto, J. (2015) *Uhakiki Linganishi wa Nduni za Mashujaa: Sakawa na Fumo Liyongo*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.
- Knappert, J. (1983) *Epic Poetry in Swahili and other African Languages*. Leiden: E. J. Brill.
- Kunene, M. (1980) “Review of the Epic in Africa: Towards a Poetics of the Oral Performance”. *Research in African Literature*, Juz. Na. 11(4): 552-559.
- Lyamuya, H. N. (2014) *Ulinganishi wa Sababu za Kuanguka kwa Shujaa katika Utendi wa Kiswahili na Tendi Nyingine za Kiafrika*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Mahenge, O. (2016) *Shujaa wa Jamii ya Wakinga*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Malangalila, F. A. (1987) *Mwamuyinga: Mtawala wa Wahehe*. Peramiho: Benedictine Publication.
- Mbele, J. (1986) “The Identity of the Hero in the Liongo Epic”. *Research in Africa Literature*, Juz. Na. 17(4): 464-473.
- Mbiti, S. J. (1969) *African Religious and Philosophy*. Johannesburg: Heinemann Publisher.
- Mofolo, T. (1975) *Chaka Mtemi wa Wazulu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mtega, W. (2017) *Uhusiano wa Taashira na Maisha ya Shujaa wa Kiutendi: Uchunguzi wa Utensi wa Rasi'lGhuli na Utensi wa Nyakiiru Kibi*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Mulokozi, M. M. (Mh.) (1999) *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mulokozi, M. M. (2002) *The African Epic Controversy*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

- Mulokozi, M. M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- Mumford, B. (1934) "Hehe-Bena-Sangu Peoples of East Africa". *American Anthropologist*, Juz. Na. 36 (2): 203-222. Inapatikana katika <https://doi.org/10.1525/aa.1934.36.2.02a00060>. Ilisomwa tarehe 4/9/2022.
- Ngassapa, D. (Mh.) (2011) *Mukwavinyika Mwamuyinga na Kabilia lake la Wahehe*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Okpewho, I. (1979) *The Epic in Africa: Towards a Poetics of the Oral Performance*. London: Longman Publisher.
- Raglan, L. (1934) "The Hero of Tradition". *Folklore*, Juz. Na. 45 (3): 212-231. Inapatikana katika <https://doi.org/10.1080/0015587x.1934.9718559>. Ilisomwa tarehe 15/10/2023.
- Samwel, M. (2015) *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: MEVELI Publisher.
- Senkoro, F. M. K. (1997) *The Significance of the Journey in Folk Tales from Zanzibar*. Tazmili ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Seydou, B. (1983) "A Few Reflections on the Narrative Structure of Epic Text: A Case Example of Bambara and Fulani Epics". *Research in African Literature*, Juz. Na. 14(3): 312-331.
- Sikuomba, B. (2018) *Mandhari na Shujaa wa Kiutendi katika Tendi za Kiswahili: Uchunguzi wa Utendi wa Fumo Liyongo na Utendi wa Nyakiiru Kibi*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Sosoo, F. (2018) *Ushujaa katika Motifu ya Safari na Msako: Ulinganishi wa Ngano za Kiewe kutoka Ghana na Riwaya za Shaaban Robert kutoka Tanzania*. Tazimili ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Sosoo, F. (2020) "Ujitokezaji wa Ruwaza ya Shujaa katika Ngano za Kiewe kutoka Ghana na Riwaya za Shaaban Robert kutoka Tanzania". *Mulika*, Juz. Na. 38: 1-25.
- Sungi, N. A. (2011) *Ruwaza ya Shujaa Mwanamke wa Kiutendi katika Jamii ya Wanyanyembe wa Tabora*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Willoughby, P., Blittner, K., Bushozi, P. na Miller, J. (2019) "A German Rifle Casing and Chief Mkwawa of the Wahehe: The Colonial and Postcolonial Significance of Mulambalasi Rockshelter, Iringa Region, Tanzania". *African Archaeology*, Juz. Na. 17(2): 23-35.
- Wright, M. I. (1961) *The Hehe*. Dar es Salaam: Institute of Current World Affairs.